**HOTUBA YA NAIBU KATIBU MKUU ENG. NADHIFA S. KEMIKIMBA KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA 12 CHA BODI YA MAJI YA TAIFA KILICHOFANYIKA TAREHE 24 JULAI, 2020 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA VETA, JIJINI TANGA**

**Ndugu Prof. Hudson Nkotagu Mwenyekiti wa Bodi,**

**Wajumbe wa Bodi,**

**Wawakilishi wa WARIDI,**

**Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo,**

**Maafisa wa Maji,**

**Wataalam,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana,**

## Habari za asubuhi!

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia kukutanana hapa leo tukiwa na afya njema. Pili, nawashukuru Wadau wetu wa Maendeleo (WARIDI) ambao wamefadhili mafunzo ya Wajumbe wa Bodi pamoja na kikao hiki wakishirikiana na Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani. Vile vile nawashukuru Sekretariat kwa maandalizi ya kikao hiki. Mwisho nawashukuru wote mliotenga muda wenu na rasilimali fedha na kuhakikisha mnashiriki kikao hiki muhimu. Nasema asateni sana.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Natambua kuwa Bodi ya Maji ya Taifa ni chombo cha ushauri kwa Mhe. Waziri mwenye dhamana ya maji katika uratibu wa sekta mbalimbali wa mipango ya pamoja ya uendelezaji wa rasilimali za maji na utatuzi wa migogoro ya Mabonde na maji shirikishi ya kimataifa. Kwa majukumu haya, Bodi hii ni chombo muhimu sana kutokana na ukweli kwamba mafanikio katika utekelezaji wa shughuli za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji yanategemea sana ushirikishwaji wa Wadau. Aidha, ni kutokana na msingi huo, Bodi hii ikaundwa na wadau kutoka sekta tofauti tofauti ili kuhakikisha

kuwa Wadau mbalimbali wanashirikishwa katika maamuzi yanayofanywa na Bodi kupitia Wawakilishi wao.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Ni ukweli usiopingika kuwa kadri maendeleo yanavyoongezeka ndivyo rasilimali za maji zinavyopungua. Hali hii inaongeza uhitaji wa kushirikisha Wadau katika kufanya maamuzi mbalimbali ya kitaifa na hata kimataifa. Ni kupitia ushirikishwaji wa Wadau vipaumbele vya taifa vitaainishwa. Aidha, kupitia ushirikishwaji wa Wadau, migogoro inayohusiana na matumizi ya maji itaweza kudhibitiwa.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Bodi yako kwa ushauri mbalimbali mlioutoa kwa Mhe Waziri ili kuhakikisha kuwa maswala ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji yanatekelezwa iapasavyo na kuleta maendeleo kwa umma. Ushauri huu ni pamoja na;

(i) Kufanya vikao vyenu kwa kutembelea Bodi za Maji za Mabonde ili muweze kuona na kujadili changamoto mbalimbali zinazokabili Bodi hizo na hatimaye muweze kushauri namna ya kutatua/ kupunguza changamoto zilizopo.

(ii) Kuwasilishwa kwa Mipango ya Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji ya Mabonde. Hii itatoa fursa kwa Wajumbe kujua mipango hii kwa undani na hatimaye kushauri namna bora ya kuboresha na kutekeleza mipango hiyo.

(iii) Kushauri namna bora ya kuboresha uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha kuwa maji yaliyopo yanahifadhiwa na yanachangia katika ukuaji wa maendeleo endelevu ya Taifa.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Mnatambua ya kuwa nchi yetu imeingia katika Uchumi wa Kati, ni wakati muafaka kwa Bodi yako kuhakikisha kuwa mafanikio haya yaliyofikiwa yanaendelea kukua kwa kasi. Aidha, ni wazi kuwa bila kuwepo kwa

upatikanaji wa rasilimali maji za kutosha, nchi yetu haiwezi kufanikiwa katika mkakati wake wa uchumi na viwanda. Hivyo nichukue fursa hii kuiomba Bodi yako, kufuatilia kwa karibu na kumshauri Mhe. Waziri namna bora ya kuhakikisha kuwa Mipango Shirikishi ya Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji (IWRMD Plans) inatekelezwa katika Mabonde yote tisa. Ni kupitia uandaaji na utekelezaji wa Mipango IWRMD katika Mabonde nchi yetu itaendelea kuwa na ukuaji endelevu wa uchumi na kuleta maisha bora kwa Watanzania wote.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Nichukue fursa hii kuwashukuru Maafisa wa Maji kwa jitihada wanazozifanya kuhakikisha kuwa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji unakuwa endelevu. Aidha, Niwakumbushe kuwa ni wakati muafaka kuhakikisha kuwa kasi ya utambuzi wa vyanzo vya maji na kuviwekea mipaka kwa ajili ya kuvihifadhi kisheria inaongezeka. Ni dhahiri kuwa mahitaji ya maji yanaongezeka kwa kasi sambamba na kuongezeka kwa idadi ya watu na kupelekea mahitaji ya rasilimali mbalimbali ikiwemo ardhi na maji kuongezeka. Hali hii inasukuma wananchi kusogea kwenye vyanzo muhimu vya maji ili waweze kufanya shughuli zao mbalimbali ikiwemo kilimo, makazi na bustani. Gharama ya kuchelewa kutambua vyanzo na kuviwekea mipaka ili vitangazwe na kuhifadhiwa kisheria itaigharimu Serikali pesa nyingi za kulipa fidia kwa wananchi. Hivyo, suala la uhifadhi wa vyanzo lipewe kipaumbele kwa maana hakuna maendeleo bila maji.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Natambua changamoto ya upatikanaji wa pesa kwa Bodi za Maji za Mabonde. Hata hivyo, changamoto hii inaongezeka kutokana na madeni makubwa ya ada za maji na Watumiaji wengine. Nitumie fursa hii kuziagiza Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kulipa madeni yao ya ada za matumizi ya maji ili kuziwesha Bodi za Maji za Mabonde ziweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kutunza, kuhifadhi, kusimamia na kugawa rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Napenda kuchukua fursa hii kukuhakikishia kuwa Uongozi mpya wa Wizara; Katibu Mkuu Eng Anthony Sanga na mimi Msaidizi wake tutatoa ushirikiano unaohitajika ili kuhakikisha kuwa Bodi inatekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, natoa tena shukrani za dhati wa WARIDI kwa kuendelea kushirikiana na sisi katika kuhakikisha kuwa sekta ya maji inatimiza matarajio ya wananchi wake kwa kuhakikisha kuwa upatikanaji wa maji unaendelea kuwa endelevu na unachangia katika kuboresha maisha ya wananchi.

**Mwenyekiti wa Bodi,**

Baada ya kusema hayo, natamka kuwa kikao hiki kimefunguliwa rasmi.